


**Toleo 5**
**Juni 2017 MILADI**
**Ramadhan 1438 AH**

**Pia Twaweza Kusimamisha Khilafah**

**Tunapinga Mpango wa Serikali wa Kuifunga HT Indonesia**

**Kura ya Maoni**

**Athari za Mvua**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta MageuziHalaqa1**

**Siasa Ya Marekani Juu Ya Mas-Ala Mawili Ya Palestina Na Iran**




# Hotubah ya Mwanachuoni Mkubwa Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah Kwa Munasaba wa Matukio Mawili: Kuanza Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Mwaka 1438 AH/ 2017 Miladia, na Uzinduzi wa Chaneli ya TV ya Al Waqiyah

**Hotubah ya Mwanachuoni Mkubwa Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**Kwa munasaba wa matukio mawili:**

# Kuanza kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Mwaka 1438 AH / 2017 Miladi, na Uzinduzi wa Chaneli ya TV ya Al Waqiyah



**Usiku wa Ijumamosi 1 Ramadhan 1438 Hijiria/ 27 05 2017 Miladia**

الصفحة الرسمية Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah - Official Page عطاء بن خليل أبو الرشتة

Sifa njema ni zake Allah (swt) na Sala na salamu zimfikie Mtume (saw), Familia yake, masahaba zake na wote wanaomfuata…

Wapendwa Waislamu, ndugu zangu wapenzi wabebaji daawa, wapenzi watazamaji na wapenzi wasikilizaji na kwa wote wenye nyoyo za unyenyekevu na wanaosikiliza kwa makini,

Asalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh,

Ndugu zangu wapenzi mabwana na mabibi, nakupeni habari njema katika usiku huu wenye baraka kwa kuadhimisha matukio mawili muhimu sana:

**Kwanza:** tukio la kujiliwa na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani:

Baada ya kufuatilia kwa makini suala la mwezi mtukufu wa Ramadhan usiku wa leo Jumamosi tarehe 27/5/2017 muandamo wake umethibitishwa na kukidhi vigezo vya kisheria katika baadhi ya Nchi za Waislamu, hivyo basi kesho Jumamosi ni siku ya mwanzo ya kuanzia mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Kutoka kwa Bukhari kutoka kwa Muhammad bin Ziyad alisema”nilimsikia Abu Huraira (ra) akisema Mtume(saw) sala na salamu ziwe juu yake na familia yake, alisema: Abu Al Qassim (saw):

«صوموا لِرُؤيتِهِ وأَفطِرُوا لرؤيتِهِ فإنْ غُبِّيَ عليكم فأكْمِلُوا عِدَّةَ شعبانَ ثلاثين»

“Fungeni kwa kuonekanwa kwa mwezi na fungueni kwa kuonekanwa kwa mwezi, na kama kutakuwepo na mawingu (yakakuzuwiyeni musiuone mwezi ) kamilisheni siku 30 za Sha’ban”

Allah (swt) kaufanya Mwezi huu Mtukufu ni mwezi wake na anawalipa wanaofunga thawabu anazozitaka, yaani thawabu zisizokuwa na idadi. Katika hadith Qudsi Mtume (saw) Anasema:

«كُلُّ عَمَلِ ابْنِ آدَمَ لَهُ إِلَّا الصَّوْمَ، فَإِنَّهُ لِي وَأَنَا أَجْزِي بِهِ»

“Amali zote za wanadamu ni zao wao isipokuwa funga ambayo ni yangu mimi, na mimi ndiye nitakayewalipa”.

Huu ni mwezi makhsusi katika tareekh ya Kiislamu, ambao ndani yake iliteremeshwa Quran Tukufu:

[شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ]

“Ni ndani ya mwezi wa Ramadhan ndio ambao imeteremshwa Quran, ili iwe muongozo kwa watu na hoja zilizowazi na upambanuzi” (wa baina ya haki na batil) (Al Baqara: 185)

Katika mwezi huu Waislamu walishindana katika kutenda mema kwa sababu matendo mema katika mwezi huu yana thawabu na ujira mkubwa zaidi, na huku wakitafuta msamaha wa Mwenyezi Mungu kwa kufunga kwa ikhlasi na kujitolea kidhati.
Katika sahihi Bukhari kutoka kwa Abu Huraira (ra) kutoka kwa Mtume (saw) amesema:

«مَنْ صَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ، وَمَنْ قَامَ لَيْلَةَ الْقَدْرِ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

*Endelea Uk..3*

"Yoyote atakayefunga mwezi wa Ramadhan kwa imani thabiti na kutarajia malipo yake kwa Mwenyezi Mungu basi atasamehewa madhambi yake yaliyopita, na yoyote atakayehuisha ibada katika usiku wenye cheo, akiwa na imani thabiti na akitarajia malipo kutoka kwa Allah basi atasamehewa madhambi yake yote yaliyopita."

Makhalifa na Mawali katika Dola ya Kiislamu walikuwa wakihifadhi usalama wa nchi na watu wake, na waliusambaza Uislamu duniani kote kwa njia ya Da'wah na Jihad. Makhalifa waliwaongoza Waislamu kwa sheria za Allah na waliwaongoza katika Jihad kwa ajili ya Allah, jeshi lao lilisafiri kupitia majangwa makubwa na joto kali, na merikebu zao zikapambana na mikondo ya mawimbi makali katika njia ya kulifanya neno la Allah liwe juu na kueneza haki na uadilifu ulimwenguni kote. Majeshi yao yakiikhutubia bahari kwa kuieleza: "Lau tungejua kama kuna ardhi yenye kukaliwa na watu nyuma yako, basi tungevuka bahari kwenda kusimamisha bendera ya Uislamu". Aidha, Makhalifa nao walikuwa wakinadi wakiyambia mawingu ya mvua: "Ewe mvua! nyesha popote utakapo, kwa kuwa popote utakaponyesheza utakayoimwagilia ni ardhi ya Waislamu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu" Waislamu walisimama nyuma ya kiongozi wao Khalifa wakimuunga mkono afanyapo mema/mazuri na wakimuhisabu anapokosea, kwani walifahamu kuwa wao na Khalifa ni sawa mbele ya sheria. Umma, serekali na jamii wote walikuwa wakiharakishwa kwa Uislamu na kuunganishwa nao. Waliikaribisha Ramadhani kwa furaha isiyo na kifani na moyo mkunjufu, na waliiaga kwa majonzi na masikitiko, na wakiomba wakutane nayo tena kwa mara nyengine, ili wapate matukufu yaliyomo ndani ya Ramadhan, kwa kupata mafanikio ya duniani na akhera, na huko ndiko kufaulu kukubwa. Tunamuomba Allah (swt) Aufanye mwezi huu uwe wa kheri kubwa na baraka tele kwa Waislamu wote, na ikifika Ramadhan ijayo tuwe tayari tunaishi ndani ya Dola ya Kiislamu ya Khilafa Rashida. Ni Khalifah ndie atakaeshughulikia suala la kuandama kwa mwezi, na ndie atakaewatangazia Waislamu kuanza kwa Ramadhan, na kuirejeshea tena Ramadhan hadhi ya kuwa mwezi wa ushindi na Jihad pamoja na barka na rehma kwa Waumini. Wakati huo Ramadhan itakuwa tena chini ya kivuli cha Khilafah, na nuru yake itarejea na kung'ara tena. Na itarejea tena kuwa mwezi wa ibada na Jihad. Na Takbir zake zote mbili zitarejeshwa ; Takbir ya Muadhini ya kutujuza muda wa kufuturu (Iftar), na Takbir za Mujahidina ikitujuulisha ushindi. Na hilo lipo karibu kwa idhini na tawfiki ya Allah Inshallah.

إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا

"Kwa yakini Allah Anatimiza kusudio lake (lolote alitakalo hakuna wa kumpinga) hakika Mwenyezi Mungu amekwisha kiwekea kila kitu kipimo chake (At-Talaq: 3)

**Habari njema ya pili** ambayo ningependa kuwafikishia ni uzinduzi wa Chaneli ya Runinga ya Al-Waqiyah ndani ya usiku huu mtukufu. Leo hii mti wa Habari wa Hizb ut Tahrir umetoa matunda yake. Umezaa matunda yenye siha na rutba yanayofurahisha macho na yanayotuliza nyoyo. Ni tunda na tija itakayolinda hadhira yake dhidi ya ghilba, uongo na upotoshaji. Itaitangaza haqi na kuifedhehi batil. Ni tunda litakaloshuhudiwa na macho na kung'arisha fikra, ni tunda litakalozaa kheri kwa hadhira yake na wote wenye nyoyo na usikivu makini. Ni tunda linaloitwa Waqiya (Mlinzi) na ni mlinzi kwa maana yake, jina zuri lilioje pamoja na maana yake. Kwa kuwa itaonesha njia na kuonesha usahihi wake kwa kushikamana na haqi na kuitangaza. Ni tunda litakaloleta kheri kwa watu wake na kwa watu wengine watakaosikiliza kwa mazingatio.

[قُلْ هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ عَلَى بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي وَسُبْحَانَ اللَّهِ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ]

"Sema hii ndio njia yangu ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa ujuzi wa kweli, nafanya (kazi hii) mimi na wanaonifuata". Na utakatifu ni wa Allah, nami sio miongoni mwa washirikina" (Yusuf: 108)

Kwa kukhitimisha, nazindua kwa jina la Allah faraja yetu hii (Al Waqiyah) ili iweze kuunganisha viungo viwili navyo ni matangazo na gazeti la Ar-Raya, ambayo vitafanya kazi bega kwa bega katika kupaza kwa nguvu taarifa za ukweli kupitia audio na video, na kupitia machapisho na video ili kusafisha uoni, kuhuisha nyoyo na kueneza kheri duniani kote pomoja na kuinua Uislamu daraja ya juu ya mifumo yote.

[أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ]

"Jee hukuona jinsi Mwenyezi Mungu alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri ambao mizizi yake ni imara na matawi yake yametandawaa mawinguni"(Ibrahim: 24)

Na mwisho wa kauli yetu tunasema: Shukran zote anastahiki Mwenyezi Mungu. Mola wa walimwengu wote.

**Wassalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu.**
**Ndugu yenu, Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
**Amiri wa Hizb ut-Tahrir**

**Jumamosi, 1 Ramadhan 1438 Hijiria/ 27 05 2017 Miladia**

# Kama Tunavyotekeleza Swaum Pia Twaweza Kusimamisha Khilafah



Alhamdulillah tupo ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ulio na neema kubwa ya ibada tukufu ya Swaum inayotekelezwa katika siku chache mno ( أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ). Waislamu wote hufunga baada tu ya kuonekanwa kwa mwezi mwandamo au kukamilika kwa siku thelathini za Mwezi wa Sha'baan. Utukufu wa ibada hii unadhihirika jinsi ya Mwenyezimungu SWT alivyo wahutubia waja wake wenye imani hutoba ya moja kwa moja akisema

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

{Enyi Mlioamini mumefaradhishiwa kwenu kufunga kama ilivyofaradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha MwenyeziMungu}

Daktour Fadhil Samurai kwenye Lamasat Bayaniyah ataja hikma ya jinsi gani Mwenyezi Mungu alivyowaita Waumini katika ufaradhi huu wa swaum. Akasema:

نلاحظ ربنا تعالى قال يا ايها الذين آمنوا ناداهم بنفسه ولم يقل (قل يا أيها الذين آمنوا) لم يخاطب الرسول وإنما ناداهم مباشرة لأهمية ما ناداهم إليه لأن الصيام عبادة عظيمة قديمة كتبها تعالى على من سبقنا فنادانا مباشرة ولم ينادينا بالواسطة

Tunakuta kuwa Mola wetu alietukuka alisema Enyi Mlioamini akawaita yeye mwenyewe hakusema (Sema.. ewe Mtume waambie waumini enyi mlioamini) Kihakika MwenyeziMungu aliwaita moja kwa moja kwa ule umuhimu wa anachowaitia na hilo ni kuwa swaum ni ibada kubwa ya zamani alioifaradhisha MwenyeziMungu kwa waliotutangulia hii ndio maana akatuita moja kwa moja wala hakutuita kupitia wasita).

Pindi tukitathmini ibada ya funga tutakuta kuwa inabeba mafunzo makubwa ambayo nyoyo na viwilili vyetu vitakuwa vimejaa nishati kubwa ya kutekeleza majukumu yetu aliyotukalifisha MwenyeziMungu SWT huku tukilenga radhi zake. Ni muhimu kuelewa kuwa shabaha pekee ya matendo ya Mwislamu ni kupata radhi za MwenyeziMungu wala sio kutafuta maslahi ya kidunia kama ilivyo kwa warasilimali.

**Athari ya faradhi inapotekelezwa na watu wengi**

Tukiangalia kwa makini tutakuta kuwa Waislamu wote wamefahamu kuwa Ramadhani ndio mwezi wa faradhi ya Swaumu. Nao kote duniani hufunga ila wale ambao wamevuliwa kisheria. Jambo hili limeathiri mpaka wasokuwa Waislamu nao utawaona wakizungumzia Ramadhani kuwa ni mwezi ambapo Waislamu hutakikana kufunga. Hapa kuna dhihirika kuwa Waislamu wanapotekeleza kwa idadi kubwa faradhi yoyote ile kikamilifu basi watu wote duniani hutambua ibada hiyo. Mara nyingi katika jamii yoyote ile ikipatikana ndani yake wengi wafanyao mema basi ni rahisi mno wafanyao mabaya kushikwa na haya. Kinyume chake jamii inayokithirisha maasi ndani yake basi inakuwa wafanyao mema nao hutekwa na ubaya wa wale wabaya. Mfano wa wazi hapa ni leo kwa kuwa twaishi katika jamii ya kisekula ilimezeshwa sumu hii basi Waislamu wamekuwa masekula! Hivyo lau faradhi ya daawa ya kuulingania sheria za Allah tunaitakeleza kama tunavyotekeleza swaum basi rai jumla ya watu duniani ingekuwa juu ya Uislamu. Ikiwa tumeweza kuathiri ulimwengu mzima kwa ibada tu ya mwezi Mmoja hali itakuaje lau kama sote twashikana katika kutekeleza faradhi ya kulingania mwito wa Khilafah na kuifanya ni kadhi yetu ya kufa kupona?

**Umoja wa Waislamu katika kutekeleza faradhi moja ni jambo lawezekana**

Tukiangalia zaidi tunaona kuwa Shia na sunni wote hukubaliana juu ya faradhi ya swaum, na kuwa ni mwezi wa Ramdhani pekee ndio swaumu huwa faradhi. Na kuwa funga ni kujizuia na vilaji na vinywaji na kutofanya tendo la ndoa - mchana wa Ramadhani, tokea alfajiri hadi magharibi kwa nia ya kiibada. Tafsiri hii ni kwa wote. Wote hao huitekeleza funga kwa kipindi maalum cha Ramadhani wala hakuna miongoni mwao anayechelewesha utekelezaji wake katika miezi mingine. Hii ina maanisha Waislamu licha ya kutofautiana juu ya mambo ya mitagaa ya Dini au hata baadhi ya mitagaa ya aqeeda , lakini inapokuja faradhi huungana kuitekeleza. Hivyo ile dhana kuwa Waislamu hawawezi wakashikana kipamoja katika kutekeleza faradhi ya kusimamisha Khilafah kwa sababu ya kuweko tofauti baina yao ni dhana potofu bali kiasili hupaliliwa tu na maadui wa Uislamu. Kwa kweli utekelezwaji wa Swaum ni nishati muhimu sana ya kupelekea Waislamu kutekeleza faradhi nyengine. Na faradhi gani ilio kubwa leo kama sio hii ya kusimamisha Khilafah ambayo kwayo Sheria za Kiislamu huweza kutekelezwa.

**Uwezekano wa Umma kuachana na fikra hatari za Kikafiri**

Kwa hakika utekelezwaji wa Swaum unadhihirisha wazi kuwa Umma wa Kiislamu bado una nafasi kubwa ya kurudi katika twaa ya Allah kwa kufuata maamrisho yake na kukatazika na makatazo yake. Na hilo ni kuwa ikiwa Waislamu wote huweza kujizuia na mambo yanayoharibu swaumu kama vile kula, kunywa, na kufanya tendo la

ndoa mchana wa Ramadhani, basi vile waweza wakajizuia na siasa za kikafiri za kidemokrasia. Je vipi isemwe kuwa umma wa Kiislamu hauwezi kuacha fikra chafu na hatari za kikafiri kama vile Demokrasia ilhali umma huu huu leo kwa mchana kutwa wa Ramdhani unajizuia na kula na kunywa sio kwa amri ya serikali bali kwa amri ya Muumba wake. Kinachohitajika ni juhudi kubwa zifanywe katika kuingiliana na Waislamu ili kuwajenga kifikra na kuwainua kiufahamu.

**Bado umma una Imani**

Kufunga kwa Waislamu na kuingia misikitini kwa wingi ndani ya Ramadhani ni bishara kuwa bado umma una uhai. Haifai kamwe kuukatia tamaa. Na yale madai kwamba Waislamu leo hawawezi kusimamisha faradhi ya Khilafah kwa hoja ya kuwa hawana imani ni madai na fikra finyu. Bali madai haya ni hatari yanayohujumu nishati ya Kiislamu. Licha ya hilo wanao dai madai hayo wenyewe wanajigonga kwani miezi michache tu kabla ya kuingia ndani ya Ramadhani hao hao huwakumbusha Waislamu faradhi ya kufunga tu pasina na 'kujenga' kwanza imani…! Mbona hawakatazi Waislamu kufunga mpaka ijengwe imani? Lakini kwa kuchanganyikiwa kwao Mola awaongoze inapotajwa mama wa faradhi Khilafah mbio husema mpaka imani kwanza….Vipi wao wanahukumu?

Haya ni baadhi tu ya mafunzo ambayo twapasa kuyazingatia kila tunapoingia mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Twamuomba MwenyeziMungu afungue nyoyo za Waumini katika Mwezi huu bora ile waweze kuwa na nishati ya kufanya kazi ya kuhuisha maisha ya kiislamu kwa kuregesha upya serikali ya Kiislamu ya Khilafah. Amiin

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vyahabari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Tunapinga Mpango wa Serikali wa Kuifunga Hizb ut-Tahrir Indonesia




**Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari**

Katika kongamano la Vyombo vya Habari lililofanyika Jumatatu tarehe 8 Mei, 2017; Waziri wa Kuratibu Masuala ya Kisiasa, Sheria na Usalama (Menkopolhukam) Wiranto alitangaza hatua za kulifunga shirika la Hizb ut-Tahrir Indonesia (HTI) kwa misingi kuwa HTI inatambulika kuwa haina mchango mwema kwa hatua za maendeleo kufikia malengo ya kitaifa; na ina ishara za wazi kuwa ipo kinyume na azma, misingi na sifa za filosopia nadharia ya utaifa (Pancasila) na katiba ya Mwaka 1945 ya Jamhuri ya Indonesia kama ilivyowekwa ndani ya Sheria Na.17 Mwaka 2013 kuhusu washiriki wengi; imefanya shughuli ambazo zimesababisha mgongano ndani ya jamii ambao unatishia usalama na utulivu wa umma na unahatarisha maadili ya Umoja wa Jamhuri ya Indonesia (NKRR).

**Kwa sababu hiyo, Hizb ut-Tahrir Indonesia inasema:**

1. Kwa nguvu zote tunapinga mpango wa kuifunga, kwani hatua hiyo haina msingi kabisa. Hizb ut-Tahrir Indonesia ni muungano unaotambulika kisheria (BHP) Na.AHU-0000258.60.80.2014 ya tarehe 2 Julai, 2014. Kama shirika linalotambulikana na sheria, HTI ina haki za kikatiba kufanya da'wah ambayo ni muhimu katika kuboresha taifa hili na serikali. Hivyo basi, haki zinastahiki kuhifadhiwa na kulindwa na serikali, na zaidi ni kuwa shughuli za HTI zimeshudiwa zikileta khair kwa watu katika maeneo tofauti ya taifa hili. Hivyo basi, mpango wa kuifunga ambao serikali imeazimia itakuwa inakiuka haki za kikatiba ambazo zinadhaminiwa na sheria zilizopo na zitaondosha wema. Na kwa mtizamo wa kisharia, kuifunga HTI ni kumaanisha kuwekea vikwazo shughuli za da'wah ambazo athari zake ni mbaya mno mbele ya Mwenyezi Mungu kesho akhera.

2. Tukizingatia zaidi ya miaka 20, HTI imeonyesha kuendesha shughuli zake za da'wah kwa mpangilio, upole na Amani kwa mujibu wa hatua zilizowekwa. Hivyo basi, shtuma dhidi ya HTI kuwa shughuli zake zimesababisha mgongano na kutishia usalama na utulivu wa

*Endelea Uk..6*


umma na kuhatarisha maadili ya Umoja wa Jamhuri ya Indonesia ni lawama za uongo.

3. Kama shirika la da'wah, shughuli za HTI ni kueneza mafundisho ya Uislamu. Hakuna kitu kinachoenezwa na HTI au kinachohusiana na Aqeedah (Itikadi ya Kiislamu), Shakhsiyyah (Siasa), Shariah (Sheria ya Kiislamu), Da'wah (Kueneza Uislamu), Khilafah (Serikali ya Kiislamu) au nyinginezo isipokuwa mafundisho ya Uislamu. Kwa mujibu wa kipengee 59 cha Sheria No.17/2013 kuhusu mjumuiko wa wengi, mafundisho ya Uislamu hayakujumuishwa katika mafundisho ya-yanayoitwa upinzani kwa Pancasila. Hivyo basi, shtuma kuwa shughuli za HTI ni kinyume na Pancasila si kweli, na ni kinyume na sheria kuhusu mjumuiko wa wengi yenyewe!

4. Kupitia shughuli za da'wah zinazoendeshwa katika kila eneo ndani ya Indonesia, HTI imechangia mchango muhimu katika maendeleo ya binadamu katika nchi hii ili kuwaruhusu watu kuwa na uchajimungu na tabia nzuri, vitu vinavyohitajika hususan tukizingatia majanga yanayoikumba nchi hii mfano ufisadi ambao umetokana na udhaifu wa maadili ya wanadamu waliopo. Napia HTI inahusika katika juhudi za kuzishtumu sheria tofauti tofauti za kiliberali ambazo zinalenga kulidhuru taifa na serikali mfano sheria kuhusu Mafuta na Gesi, Rasilimali Asili, Uekezaji, Natioanal Education na nyinginezo ikiwemo; dhidi ya madawa ya kulevya, dhidi ya harakati za kujitenga. Wanachama wa HTI walijitolea katika kuwasaidia wahanga wa mikasa katika maeneo tofauti tofauti mfano Aceh tsunami (2004), mtetemeko wa ardhi wa Jogjakarta (2006) na mengineyo. Hivyo basi, shtuma dhidi ya HTI kuwa eti hatuna mchango mwema ni urongo.

5. Kutokana na nukta hizo hapo juu; HTI inaitaka serikali kusitisha mpango wa kuifunga Hizb ut-Tahrir Indonesia. Ikiendelea Umma utakuwa na ushahidi kuwa serikali iliyoko mamlakani iko dhidi ya Uislamu na ni katili. Hoja ni kuwa hapo nyuma baada ya kuwapiga vita Ulemaa na ambao wengine wameshikwa mpaka sasa, kisha kufunga au kuweka kikwazo kwa shughuli za da'wah katika maeneo fulani na sasa kuchukua hatua za kuyavunja mashirika ya Kiislamu. Ilhali wakati huo huo serikali iko kuwalinda wanaoikashifu Qur'an ikiwemo kupitia mahakama ambazo hazina zinazopendelea wazi na zinzoshuhudiwa na umma. Hasbunallah wa ni'mal wakiil, ni'mal maula wa ni'man nasiir.

**Muhammad Ismail Yusanto**
**Mzungumzaji Rasmi wa**
**Hizb ut Tahrir Indonesia**



# Kura ya Maoni



Kura ya maoni ni mbinu ambayo hutumika kufanyia utafiti ili kupima muelekeo wa watu juu ya jambo fulani, ama kupima umaarufu wa mtu fulani akilinganishwa na watu wengine. Mbinu hii ya maoni ya watu juu ya jambo au mtu fulani, ni ya kawaida kutoka zamani na asili yake ni mubah wala haifungani na mfumo au nidhamu yeyote.

Mbinu hii inapotumika vizuri (kwa ikhlas) ina uwezekano mkubwa wa kutabiri au kupeana taswira ya hali halisi ya matakwa ya wengi yanavyoelekea. Pia kinyume chake yaweza kutumika kuhadaa watu juu ya hali halisi ya mambo.

Kuna mambo manne (4) msingi ambayo yasipozingatiwa huathiri kura hii ya maoni na kutoa utafiti wa makosa.

**Swali** -linaloulizwa lazima liwe moja na lenye kueleweka kwa watu wote.
**Mahali/Eneo** -patakapofanyika utafiti huo pana mchango mkubwa juu ya matokeo.
**Mbinu/Ala** –zitakazotumika katika kura hiyo ya maoni.
**Muda/Wakati** –ambao itafanyika kura ya maoni hayo.

Kwa umuhimu wa mbinu hii leo imekuwa mbinu kuu ambapo kuna mashirika kadhaa ulimwenguni yamejitolea muda na rasilimali zao kuhakikisha tu wanafanya utafiti juu ya maoni ya watu fulani wanaogombea nyadhifa fulani za uongozi. Utashangaa kwa mashirika haya namna yanavyotia bidii juu ya jambo hili hususan kunapokaribia uchaguzi.

Leo hapa Kenya kuna mashirika kadhaa yanayo jihusisha kufanya utafiti juu ya maoni ya watu ili kubainisha ni nani kati ya wagombeaji aliyen a umaarufu zaidi akilinganishwa na mwengine. Kuna mashirika kama vile IPSOS, INFOTRACK na mengineo ambayo mara kwa mara utoa utafiti wao na kutabiri maoni ya watu yanapendelea nani.

Tukizingatia ya kwamba leo ulimwengu mzima twaishi chini ya mfumo wa kirasilimali, basi kwa njia moja au nyengine mashirika haya yametekwa na kubebwa na mfumo huu bali yamerasilimanishwa na tafiti zao zimekuwa ni za kimrengo, ima kupaka mafuta mrengo fulani au

*Endelea Uk..7*

kuporomosha upande wa pili.

Hili limedhihirika pale shirika la maoni la IPSOS linapomueka Uhuru Kenyatta kifua mbele kila linapofanya utafiti wake licha ya hali ngumu za maisha na ufisadi ulio juu katika serikali yake. Shirika hili hujaribu kuficha aibu ya serikali wakati ambapo wanahisi serikali iko katika hali ngumu zinazodhihirisha kuchoshwa kwa raia wake.

Nyakati hizi aghalabu wao ndio hutoa tafiti zao na kuipigia debe serikali. 23 Disemba, 2016 baada ya mgomo wa walimu wa takriban mwezi mzima ulio athiri sekta ya elimu Kenya nzima ambapo watu walikemea serikali kwa kuzembea juu ya majukumu yake, Lakushangaza bado shirika hilo lilimueka Uhuru Kenyatta kifua mbele kwa umaarufu kwa asilimia 75% juu akilinganishwa na wengine! Licha ya balaa zilizozuka katika sekta hiyo ikiwemo msururu wa kuchomwa kwa mashule, kashifa za ufisadi wa NYS na utovu wa usalama jumla.

Mwezi wa Januari, 2017 ulioshuhudia mgomo wa madaktari kwa takriban miezi mitatu na kuleta maafa Kenya nzima, ambapo serikali ya Uhuru ililifumbia macho suala la madaktari bali waliwatisha kuwafuta kazi na hata wakathubutu kuwatia mbaroni viongozi wa muungano wao, jambo ambalo lilimchukiza kila mkenya. Vivyo hivyo shirika la IPSOS tena lilitoa utafiti wake na kama kawaida likamuorodhesha Rais Uhuru Kenyatta nambari moja. Hii yadhihirisha unafiki wa mashirika haya kwamba tafiti zao si za kweli na hazistahiki kutegemewa!

Urasilimali huu wa kulazimisha watu ajenda si hapa Kenya tu bali hata baba wa urasilimali Marekani anaedai kujali maoni ya wengi na kulinda demokrasia ilidhihirisha unafiki wake pale walipo kataa kuheshimu maoni na hata maamuzi ya mwisho ya raia wake katika Chaguzi za Novemba, 2016. Kutoka mwanzo mashirika mengi ya kura za maoni yaliuweka mrengo wa Clinton kifua mbele akilinganishwa na Trump na hata baada ya Hillary kujikusanyia kura nyingi za maamuzi hakupewa bendera ya kuongoza Marekani, bali walipinga si tu kura za maoni bali hata kura zenyewe za maamuzi na badala yake wakamtangaza Donald J. Trump kuwa ndiye mshindi na kutawazwa kama raisi wa Marekani. Jambo ambalo lilizusha rabsha na maandamano ya kupinga ushindi wa Donald J. Trump. Hii yadhihirisha si maoni ya wingi wa watu ndio huchukuliwa bali ni warasilimali wachache ndio wanao amua nani afaa kutawala pasi na kujali demokrasia na maadili yake.

Miaka kadhaa nyuma Marekani ilipoanza kuzorota kimfumo ilipelekea raia wake na hususan wa mataifa ya Mashariki ya Kati na Afrika jumla kuchoshwa na sera na siasa zake Ulimwenguni. Hilo lilisababisha Marekani kujaribu kupaka rangi mfumo wake kwa kumbandika Barrack Obama mamlakani kimakusudi ili walete ajenda mpya ulimwenguni kwa kumtawaza mtu mweusi kama raisi  kwa taifa kuu kama Marekani. Hapa walihisi kuna umuhimu wa kuonesha ulimwengu eti wao ni wana demokrasia waliomakinika wala hawajali rangi na ukabila.

Kupitia kura za maoni kwa kweli walifaulu pakubwa kwa propaganda hii na wakauyumbisha ulimwengu mzima hususan Afrika kwamba Amerika ndio kiigizo na wakasifiwa kila upande na kiasi fulani wakafutilia mbali baadhi ya machukivu ambayo watu walikuwa wamebeba dhidi yao. Ikabaki kila mtu aimba jina la Obama kiasi kwamba wimbo ukatungwa kuwa Ikulu itapakwa rangi nyeusi kwa mara ya kwanza katika historia ya Marekani! Leo ingekuwa ni propaganga kubwa kwa mfumo wao lau wangemchagua na kumtawaza mwanamke kama raisi kwa taifa kuu kama hili na wangefaulu kulazimisha mambo mengi ikiwemo kupewa fursa wanawake kuwania nyadhifa za uongozi kilimwengu na hususan katika mataifa ya Kiisilamu. Juu ya hivyo hawakuona umuhimu huu wa kupigia debe mfumo wao kwa kumtawaza mwanamke bali walipitisha maslahi yao mbele kuliko ya mfumo wao. Hapa hawakujali kumtawaza mtu ambaye ni mtovu wa maadili, mwenye sera iliyochukiza watu na kampeni za kimataifa.

Yote hayo yadhihirisha kwamba siku zote warasilimali hawajali maslahi ya mfumo wao bali hulenga maslahi yao ya kimada wanayaona wanapopima ni nani kati ya wagombeaji ambaye atayatekeleza sera zao ili kuwawezesha kuyafikia maslahi yao kwa wepesi na uzuri Zaidi. Hapa ndio wakaamua kumpitisha mbele Donald J. Trump kwa maslahi wanayoyajua na kuyaona wao zaidi yatapatikana kupitia mtovu huyu wa maadili mwenye kauli za kifidhuli. Kwa hiyo si maoni ya wengi yenye kuzingatiwa wala maamuzi ya watu.

Tumetangulia kusema ya kwamba mbinu hii ni ya zamani wala sio mpya na inapotumika vyema (ikhlas) basi moja kwa moja husaidia pakubwa kuelekeza watu wapi asili ya maoni ya wengi wao yanapoelekea.

Katika historia ya Kiislamu ilidhihirisha vipi kura hii ya maoni ilivyosaidia kutoa muelekeo na kuwapa Waislamu chaguo bora la rai ya wengi iliobebwa asilimia ya juu ya maoni ya watu. Pindi Abu Bakr (ra) alipohisi ugonjwa wake utampelekea mauti na upande wa pili jeshi la Waisilamu la pambana na Dola mbili kubwa zama hizo Fursi na Rumi, aliwaita Waislamu na akawashauri juu ya maoni yao kwamba ni nani atakaye chukua khatamu za uongozi baada yake. Licha ya ugonjwa wake aliwauliza na kutafuta maoni ya watu kwa takribani miezi mitatu na alipopata jawabu la nani anaependelewa na watu yaani maoni ya wengi yalipoangukia kwa Umar (ra) hapo akawatangazia Waislamu kwamba Umar (ra) ndiye atakaye kua kiongozi baada yake. Na kweli ikawa ni rai ya asili ya maoni ya wengi ndio pale alipokufa Abu Bakr (ra) waisilamu kwa moyo mmoja wakampa baiya (kiapo cha ahadi ya utiifu) Umar (ra)

Pia baada ya Umar (ra) kudungwa kisu akiwa katika Swala  baada

Endelea Uk..8

ya muda maswahaba walipoona hali yake inazidi kudhoofika walimlazimisha awachagulie kiongozi baada yake. Kama historia inavyoeleza Umar (ra) aliwachagua watu sita wachaguane baina yao na akatoa muda wa siku tatu (3) baada ya yeye kufa. Abdulrahman bin Awf (ra) alichukua jukumu la kutafuta maoni ya watu juu ya nani apendekezwa zaidi katika watu watano waliobakia. Abdulrahman (ra) alilibeba jukumu hili la kura ya maoni kwa kujitolea katika upeo wake wa mwisho kabisa. Abdulrahman (ra) aliingia kila nyumba akauliza wake kwa waume juu ya nani anaependekezwa zaidi katika wale wagombeaji. Na ikatokea ya kwamba maoni ya wengi yaliangukia kwa Uthman (ra) na Ali (ra) na kazi hii aliifanya usiku na mchana kama vile Ibn Kathir alivyoeleza katika kitabu chake cha Al-Bidaya Wal Nihaya kwamba Abdulrahman (ra) alimtembelea Al–Musawar bin Makramah (ra) akamwambia **"Wallahi sijalala siku tatu"**

Yaani alitafuta maoni usiku na mchana. Na hata baada ya kupata maoni ya wengi ya watu hakutosheka bali alitaka kujua pia maoni ya hao wagombeaji akawauliza kama si wewe ni nani waona yuwastahiki Uongozi? Na hapo vile vile maoni yakaangukia Uthman (ra) na Ali (ra) huu ndio uhodari aliotumia ili kuhakikisha atapata asilimia ya juu katika maoni ya watu. Na ndio pale hata baada ya kumtanguliza Ali (ra) na baadae kumtawaza Uthman (ra) watu wote waliridhika hata Ali (ra) mwenyewe akawa mstari wa mbele kumbaisha (kutoa kiapo cha ahadi ya utiifu) Uthman (ra).

Hivi ndivyo Waislamu wanavyo beba mambo yao kwa kuhisi majukumu wala si maslahi kama inavyodhihirishwa kutoka katika mfumo batil wa kirasilimali katika mambo yake ulimwenguni.

**Hajj Salim**

# Athari Za Mvua Ni Matokeo Ya Ufisadi Nchini



Mvua inayonyesha Mombasa imesababisha maafa mengi ikiwemo Mafuriko, nyumba kusombwa na maji na pia mauti. Walioathirika zaidi ni watoto wadogo na wanawake. Nyumba zinajiporomokea kwa kushindwa kuhimili nguvu ya maji ya mvua. Maafa haya yaliyosababishwa na mvua ya mfululizo inayoendelea Mombasa, tunasema ni Qadhaa ya Allah lakini pia uzembe wa viongozi umechangia kwa kiasi kikubwa.

Ufisadi unaoendekezwa kuanzia juu kwa viongozi mpaka nchini kwa raia ndio chanzo cha maafa haya. Watu kuuza na kuuziwa au kununua shamba na kujenga sehemu pasipostahili kujengwa, ilimradi tu amepapata kwa pesa ndogo. Wenye majumba na viwanja hawataki kujua bora pesa yao inaingia kila mwezi. Watu walioko katika sekta ya ardhi nao pia hawafuatilii kesi hizi kwa sababu huwa wamenyamazishwa kwa njia moja au nyengine kupitia hongo.

Kwa kweli nchi ya Kenya imejisahau na kudidimia katika giza la mfumo wa kirasilimali na nidhamu yake ya Kidemokrasia mpaka wakashindwa kutambua kama wanafanyiwa kusudi. Ni majuzi tu watu walikuwa wanalilia njaa, ukame na joto jingi. Kwa nini Allah (swt) anatuletea rehma ya mvua tunaiwacha inamwagika kiasi cha kuleta mafuriko na kuleta maafa katika maisha ya wanadaamu. Ndipo pale tunaposema kuwa mfumo fisidifu wa Kirasilimali na nidhamu zake ikiwemo Demokrasia umezorota na haujiwezi tena kwa kushindwa kuwaongoza binadamu na kutatua matatizo yao. Viongozi wana uwezo wa kudhibiti hali hii lakini kwa ufisadi na uzembe walionao wameshindwa kabisa!

Mvua hii inayoendelea kunyesha ni funzo kwetu sisi wananchi. Funzo tunalojifunza ni kuwa Demokrasia haifai kiutawala na kuendesha maslahi ya umma? Mvua hii itatufungua macho kuangalia suluhu la kudumu au daima tutabakia kutijia hamnazo na kuotesheana vidole vya lawama? Kwa hakika wengi wetu wanawake bado hatujafahamu kama matatizo katika

*Endelea Uk..9*




Email: uqab@hizb.or.ke

ummah yanasababishwa na mfumo huu fisidifu. Ukame, njaa, kiu, mafuriko n,k yote haya ni sababu ya udhaifu wa sheria zilizotungwa na mwanadamu. Ambazo kila kukicha zinatoa mwanya wa watu kufuja pesa za umma na kukithirisha ufisadi kiasi kwamba inapelekea miundo mbinu kutelekezwa na hatimaye kusababisha maafa na hasara kubwa kila msimu.

Viongozi hawashtushwi na maafa na hasara iliyowakumba raia bali wanazunguka huku na kule wakitafuta watu wa kuwapigia debe na kuwapigia kura siku ya uchaguzi mkuu. Upande mwingine wakinyoosheana vidole vya lawama kati ya serikali na upinzani; na wengine wakitoa ahadi hewa zisizoingia akilini ikiwemo pamoja na kuwa eti watu waendelee kupata maafa tukisubiri viongozi au chama fulani kichukue mamlaka ndio watatue! Hili linadhihirika pale kina mama wanapochukuliwa na kuandikishwa majina nyumba baada ya nyumba na kuahidiwa visenti ambavyo hata haviwatoshelezi mlo wao wa siku moja. Mpaka lini kina mama tutakubali kutumiwa na kunyanyaswa na wanaDemokrasia? Ni wakati sasa tuzindukeni tutafute suluhu ya kudumu ya matatizo ya umma na mfumo mbadala ambao utatuhakikishia utulivu katika maisha yetu, watoto wetu na waume zetu.

**Mgeni J Salim**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 1: Kuanza kwa Da’wah ya Mtume Muhammad (saw)

Baada ya wahyi kumshukia Mtume (s.a.w) na kukalifishwa kubeba Risala na kuamrishwa kuifikisha kwa kauli zake Taa’la:

يأيها المدثر قم فأنذر

**“Ewe uliejifunika funika simama uonye”**
**[Al-Muddaththir: 1 – 2]**

وأنذر عشيرتك الأقربين, واخفض جناحك لمن اتبعك من المؤمنين ,فإن عصوك فقل إني بريئ مما تعملون

“Na uwaonye Jamaa zako wa karibu, Na uinamishe bawa la unyonge kwa watakaokufuata miongoni mwa waumini, Wakikuasi basi sema Hakika yangu mimi niko mbali na mnayoyatenda”
[Ash-Shuaraa: 214 – 216]

يا أيها الرسول بلغ ما أنزل إليك من ربك وإن لم تفعل فما بلغت رسالته والله يعصمك من الناس إن الله لا يهدي القوم الكافرين

“Ewe Mtume!Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na usipofanya hivyo (ukafupisha katika ufikishaji na ukaficha kitu) Basi utakua hujafikisha Ujumbe wake (utakua umefanya dhambi kubwa) Na Allah atakulinda kutokana na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu Makafiri (hawaafiqii kwa kheri wala uongofu”
[Al-Maaidah: 67]

Akawa Rasulullah (s.a.w) anawalingania watu kwa dini ya Allah (swt), akiwa ni mwenye kupambana, anaiamini Haq anayoilingania, na kutangaza vita (mvutano wa kifikra) kwa mwekundu na mweusi; pasi na kupiga hesabu zozote kuhusu mazoea ya watu, dini zao, mila zao ma hata imani zao. Kwani yeye hakujali chochote isipokua Risala ya Uislamu pekee.

Rasulullah (s.a.w) aliwalingania watu kumuabudu Allah (swt) peke yake, kujifunga na Itikadi (Aqqedah) ya Uislamu peke yake na kuzitekeleza hukmu zake katika nyanja zote za kimaisha. Pia alipambana na makafiri na washirikina dhidi ya imani zao na kuzibomoa. Aliyafanya yote hayo ilhali akiwa mtu mmoja peke yake, hana msaidizi wala silaha, isipokua imani yake iliyomakinika ndani juu ya Allah (swt) na kwa Uislamu ambao anaulingania kikamilifu.

Da’wah yake Rasulullah (saw) ilipitia Nukta (Marhala) tatu msingi nazo ni

1. Marhala ya Kwanza: kusomesha na kupeana Thaqafa
2. Marhala ya Pili: maingiliano na Ummah
3. Marhala ya Tatu: Kuchukua uongozi na kusimamisha Dola ya Kiislamu

**Itaendelea katika UQAB Toleo la 6; In Shaa Allah**

# SWALI/JAWABU: Siasa Ya Marekani Juu Ya Mas-Ala Mawili Ya Palestina Na Iran




**SWALI:**

Katika jibu la swali lilopita la 05/02/2017, imefafanuliwa misingi mikuu ya siasa ya Trump kuelekea kutumia “matunda” ya siasa ya Obama katika Syria na hasa kuibuka kwa dori ya Uturuki kwa nguvu katika kuisalimisha Aleppo kwa serikali, na vilevile kuelekea kuidunisha dori ya Urusi. Na vile vile kuelekea Marekani kuipa Uingereza dori kiasi fulani nchini Syria…Lakini kuna mambo mawili hayakutajwa, pamoja na kwamba kauli za Trump zilikuwa kali juu ya mambo hayo! Rais wa Marekani, Trump, siku ya 15/02/2017 alitoa kauli katika mkutano na waandishi wa habari alioufanya pamoja na waziri mkuu wa kijidola cha kiyahudi mjini Washington zinazohusiana na ‘utatuzi wa dola mbili’(two-state solution) kwamba yeye baada ya saa hatoendelea nalo suala hilo. Je Marekani imeliacha suluhisho hili? Na vile vile tangu Trump ashike madaraka ya urais wa Marekani tarehe 20/01/2017 kauli za Trump kuelekea Iran zimekua kali na kuifanya hali tete zaidi kuelekea upande(wa Iran). Je haya ni katika mabadiliko ya siasa ya Marekani kuelekea upande wa dori ya Iran baada ya kuwa dori hii ni kuitumikia Marekani katika eneo? Walakash-shkru.

**JIBU:**

Tutachunguza mas-ala haya mawili yaliyotajwa ili ibainike kwetu rai yenye nguvu katika mas-ala hayo mawili kwa idhini ya Allah.

**LA KWANZA: MAUDHUI YA PALESTINA AU VILE WANAVYOIITA KADHIA YA MASHARIKI YA KATI:**

1-Hakika maneno ya kauli alizozitoa rais wa Marekani Trump kama zilivyonukuliwa na vyombo vya habari vya kimataifa na kieneo vyote na kama zilivyonukuliwa hewani moja kwa moja ni : “Rais wa Marekani Donald Trump Jumatano aliandika mtzamo mpya katika siasa ya Marekani kuelekea mashariki ya kati baada ya kuthibitisha kwamba suluhisho la dola mbili sio njia pekee ya kumaliza mzozo wa Izrail-Palestina, akiashiria kwamba yeye yuko wazi juu ya badili(kadhaa) ikiwa zitapelekea kwenye amani. Na walikuwa marais wote waliopita wa Marekani wakililinda suluhisho la dola mbili, wakiwa ni kutoka Republican au Democrat”(France 24, 16/02/2017). Na akasema “Naangalia sulhisho la dola mbili na suluhisho la dola moja (…), ikiwa Izrail na Wapalestina watafurahi nami nitafurahi kwa (suluhisho) ambalo wanatalipendelea. Masuluhisho yote mawili kwangu ni sawa”(Aljazeera live,16/02/2017).

Na suluhisho la dola moja ambalo Marekani imelitaja kwa mara ya kwanza katika kinywa cha Trump, Trump hakufafanua, kuwa je ina maana kuwapa Wapelestina utawala wa ndani katika dola moja ya kiyahudi?! Au ina maana dola ya kisekula kwa kushiriki Wapelstina katia uongzi wa dola ya kiyahudi, jambo ambalo linafanana na mpango wa Muingereza ambao Uingereza iliudhihirisha mwaka 1939 ilipotoa ‘kitabu cheupe’ cha muktadha wa Lebanon? Ikieleweka kwamba mpango wa suluhisho la dola mbili ni mpango wa Marekani yenyewe ambao iliudhihirisha tangu

Endelea Uk..11

mwaka 1959 wakati wa rais wa Republican Eisenhower na ikafanya kile kinachoitwa jumuia ya kimataifa iukubali, na ikatupa suluhisho la dola moja ambalo lilileltwa na Uingereza.

Na vyovyote vile iwavyo, jambo linalodhihiri kwa mwenye kuzingatia kauli hizi na vidokezo vyake ni kuwa Marekani haijauacha mpango wake wa suluhisho la Dola mbiili, kwasababu balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa Nicky Healy alithibitisha kwa kusema: "Awali ya yote, suluhisho la dola mbili ambalo tunaliunga mkono. Mtu yeyote anayesema kwamba Marekani haiungi mkono suluhisho la dola mbili, hili litakuwa ni kosa… Kwa msisitizo tunaunga mkono suluhisho la dola mbili, lakini pia tunatafakari nje ya boksi…na ni jambo linalohitaji kuzishawishi pande mbili hizi kuja kwenye meza(ya majadiliano) na ndio tunalolihitaji ili tuzifanye ziwafikiane" (Reuters, 16/02/2017).

Hili linathibitisha kwamba Trump hajaliacha suluhisho la dola mbili. Na hii ndio siasa ya siasa ya Marekani iliyojifunganayo idara zote tangu tarehe ile tuliyoionesha. Lilipo ni kwamba alitaka kujaribu mbinu nyengine ya shinikizo, kwasababu balozi wake katika umoja wa mataifa amethibitisha kuwa nchi yake imeshaika suluhisho la dola mbili, isipokua yeye alifikiria kutumia mbinu nyengine. Au kuna marekebisho Marekani inataka kuyapitisha juu ya suluhisho la dola mbili ili adhihirike mwenye mvuto zaidi kwa Mayahudi. Na balozzi ametaja kwamba wanfikiria nje boksi, yaani ameufananansha huu machakato na boksi ambapo ilikuwa nchi yake ikizikusanya pande mbili ndani ya boksi ili kulifanyia kazi suluhisho(la dola mbili). Na anataka kutumia mbinu nyengine kwa kuzidisha au kupunguza mambo mengine yanayohusiana na suluhisho(hili la dola mbili) ili liwe na mvuto kwa wadau hasa mayahudi…

Na tofauti za mbinu hili jambo lipo. Tulitaja katika jibu la swali 18/11/2016 kuhusu siasa ya Trump baada ya tangazo la ushindi wake kwamba hakutokua na mabadiliko katika misingi ya ya siasa za marekani isipokuwa katika misingi tu. Tulisema "Ama kuhusu kubadilika kwa siasa za Marekani katika mambo ya msingi yaliyokuwepo katika kipindi cha rais ilyetangulia, kwa hakika misingi mikuu haitarajiwi kubadilika. Ni mbinu ndizo ambazo zinaweza kubadilika. Kwani serikali ya Marekani inaongozwa na asasi kadhaa na kila moja ina nguvu amabazo huzidi au hupungua. Kwa mfano, rais na ofisi yake, Pentagon, Congress, Baraza la usalama wa taifa,na idara za usalama… Zote hizi zina ushawishi katika kuhifadhi misingi mikuu ya siasa za Marekani kwa namna thabiti ijapokuwa hutofautiana katika mbinu…"

2-Mamlaka ya Palestina imeonyesha kushangazwa na kustushwa. Alisema Saeb Erekat, mapatanishi wake mkuu na wayahudi kwa muda mrefu na katibu wa kamati kuu ya PLO "Tunaamini kwamba kuharibu suluhisho la dola mbili si suala la utani lakini ni maafa na msiba kwa kila mmoja Wayahudi na Wapalestina"(Huffington Post, 16/2/2017). Na akasema Erekat: "Badili(jambo jengine) pekee la suluhisho la dola mbili ni nchi moja ya kidemokrasia na haki sawa kwa wote Waislamu, Wakristo na Wayahdi" (Aljazeera,16/2/2017)

Mamlaka na wakereketwa wake hawaelewi ila suluhisho zinazotolewa makafiri wakolni. Ikiwa si suluhisho la Marekani la dola mbili, basi itakuwa ni kurejea kwenye suluhisho la Muingereza la zamani au linalofanana nalo chini ya utawala wa Yahudi. Na inadhihirika kuwa Marekani haijawasiliana na mamlaka(ya Palestina) na wakereketwa wake kuhusu mipango yake. Na wao ni wa mwisho kujua kwani hawana thamani yoyote kwao. Kwasababu (Marekani) injaua kwamba watanyenyekea na watafuata. Kwani mwenye kutoa 80% ya ardhi yake na akaridhia kuwa awe mlinzi wa waporaji na kuwapiga watu wake katika njia ya kumlinda adui wao. Kwa hiyo huzingatiwa kuwa wa chini kabisa kupewa thamani. Hubweka kama mbwa kwa anaemtupia mfupa!

3-Ama msimamo wa kijidola cha Wayahudi, ijapokuwa waziri mkuu wake Netanyahu amemuomba rais wa Marekani na hata kwa kusaidia kwake kijidola(cha Wayahudi), lakini hakutaja chochote kuhusu mpango wa suluhisho la dola mbili katika mkutano wake na waandishi wa habari pamoja na Trump, kwa hali hiyo inadhihirika kwamba yeye hana raha kutokana na kauli za Trump. Kana kwamba kuna mambo alitakiwa na hakuridhika nayo akaona bora asiyataje ili asiondoe matarajio ya wafuasi wake Mayahudi waliyokuwa nayo kwa Trump…
Na ni wazi kwamba matakwa yake hayakufanikiwa na hakutak kudhihirisha hilo (Na aliulizwa Netanyahu kama aliigusa kadhia ya Golan akajibu "Ndio" Na alipoulizwa kuhusu jibu la rais wa Marekani, Netanyahu alisema; si semi kwamba alistushwa na ombi langu na hakuongeza ufafanuzi zaidi" (Reuters Arabic, 16/2/2017).

Na wala si kuuhamishia ubalozi wa Marekani Al-quds kama alivyoahidi katika kampeni zake za uchaguzi. "Trump alisema siku ya Jumapili kuwa mawasiliano ya simu na Netanyahu yalikuwa "mazuri, na hayo ni katika hotuba baada ya White House kufichua kwamba ipo katika "hatua za awali" za mazungumzo illi kutekeleza ahadi ya rais ya kuuhamisha ubalozi wa Marekani ndani ya Izrail kutoka Tel Aviv kwenda Al-quds. Na msemaji wa White house, Sean Spicer, akaeleza katika tamko "Tuko katika hatua za mapema mno katika mazungumzo ya suala hili". Na akasema kuwa hakuna tangazo la karibu kuhusu kuhamisha ubalozi, amabayo ni hatua itakayolipua ghadhabu zinazotarajiwa katika ulimwengu wa Waarabu.(Sky News Arabic, 22/1/2017).
Netanyahu akaona bora atie mkazo kuupiga vita Uislamu unaotishia kijidola cha Wayahudi, akasema: "Waziri mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alithibitisha utayari wake ili kuisaidia Washington

Endelea Uk..12

kupambana na "Uislamu wa siasa kali" na kuumaliza" (Gulf Online, 15/2/2017)… Wao husema "Uislamu wa siasa kali" kama sababu na kisingizio ili kuupiga vita Uislamu ambao ameuteremsha Allah Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima juu ya Mjumbe wake mkarimu(SAW). Uislamu ni ule Uislamu unaofaa kwa kwa tatizo la umma, nao ni haki (Basi nini baada haki isipokuwa upotevu? Vipi nyinyi mnapotolewa?) Yunus:32

**LA PILI: MAUDHUI YA IRAN:**

**Siasa Ya Marekani Kuelekea Iran Kabla Ya Trump:**

1-Katikati ya vita vya Marekani dhidi ya Iraki, iliitumia Iran ushawishi wote mpaka ulipomakinika utawala wa Marekani dhidi ya Iraki. Makundi matiifu kwake(Iran) yakawa hayapigani na Marekani katika wakati ambapo majimbo ya kaskazini na magharibi ya Iraki yanawaka moto, (majimbo) ambayo hakuna ushawishi wa Iran humo. Na mipangilio baina ya Marekani na Iran katika Iraki ipo katika nyanja zote na utekelezaji unafanyika kiukamilifu. Na hakuna anaeghafilika na haya ila kipofu… Na pia katika Yemen Iran inawasaidia Houthi. Na wajumbe wa kimataifa wa Marekani (wa zamani Jamal bin Umar na wa sasa Walid Al-Shaykh) ndio wanaojaribu kuliimarisha jukumu lao katika utawala wa Yemen.

Na wao Houthi ndio aliokutana nao waziri wa mambo ya nje Kerry nchini Muscat mwishoni mwa 2016, pamoja na kwamba wao ni kama Iran ambayo hunyanyua miito "Shetani mkubwa", wao hunyanyua miito "Kifo kwa Marekani". Basi dori ya Iran nchini Yemen ni dori inayotegemewa na Marekani kikamilifu… Na nchini Syria picha iko wazi kuliko jua, kwa kule Iran yeye mwenyewe na wanamgambo wake kumpa mwega Bashar, na muungano wa kimataifa wa Kimarekani unayashambulia mapinduzi nchini Syria na wala hawashambulii ISIS tu, kwa hakika wanashambulia kwa mabomu makundi kadhaa na kuua viongozi wao. Yote hayo chini ya kisingizio cha ugaidi. Na ndege za Marekani hazishambulii kundi la Iran la Kilebanon(Hizbullah) ijapokuwa kijeshi linainishwa kigaidi.

Basi dori ya Iran nchini Syria ni sehemu ya siasa ya Marekani… Kisha Marekani – Obama ametia saini makubaliano ya nyuklia ya Iran pamoja na nguvu za kimataifa Juni 2015. Marekani ilitaka kulegeza vibano, uzito na vikwazo dhidi ya Iran ili iweze kutekeleza mahitaji yanayoongezeka kwa ajili ya siasa ya Marekani katika eneo(Mashariki ya Kati) na hasa baada ya mapinduzi ya "Vuguvugu la Warabu" na kuiwezesha Iran kusafirisha nje mafuta yake na kufanya matumizi kwa ajili ya mahitaji ya siasa ya Marekani nchini Yemen, Syria na Lebanon…Na hivi ndivyo mambo yalivyo, basi yale yaliyokuwa yakisikilikana kaika kauli za Marekani dhidi ya Iran tangu mapinduzi ya mwaka 1979, na kauli kali zaidi za Iran dhidi ya Marekan, akaiita "Shetani Mkubwa", yote hayo ni maneno yanayopeperushwa na upepo. Matendo na siasa za kiutekelezaji zenye kuratibiwa kikamilifu baina yao vina ukweli zaidi kuliko vitabu vya kauli na maneno yachoshayo. Na siasa hufahamika kutokana na vitendo na si kauli tu.

2-Uongozi wa Obama umekwenda mbali zaidi kuliko uongozi wowote mwengine wa Marekani tangu mapinduzi ya Iran katika kuiachia Iran juu ya nchi zilizoizunguka. Kikadhihiri kile kilichokuja julikana kuwa "Dori ya Iran" nchini Yemen na Syria na zaidi pia Irak na Lebanon. Na kwa kuzingatia Marekani kuiongezea na kuipa umuhimu dori ya Iran tutagundua kwamba hayo yalikuwa yamesukumwa na misukumo ya Washington ya zamani na ya mipya, kama ifuatavyo:

a-**Misukumo Ya Zamani**: Nayo ni kuifanya Iran izidishe vitisho kwa mataifa ya Ghuba ili Marekani idhibiti visima vya mafuta. Na huu ndio mtazamo wa kale wa Marekani kwa dori ya Iran, ilikuwa ni kuimakinisha Marekani kwa kutia mguu katika Ghuba, yaani kwenye visima vya mafuta. Lakini kwasababu ya uvamizi wa Irak dhidi ya Kuweit mwaka 1990, Marekani imepata sababu zisizokuwa Iran kuiunganisha kwenye visima vya mafuta kwahiyo Marekani imeweza kuutumia uvamizi huu kwa kuweka kambi zake za kijeshi katika nchi kadhaa za Ghuba. Kwahiyo vitisho vya Iran vimetoweka kwa Marekani kutokua na haja navyo katika upande wa mafuta.

Baada ya kupata uongozi wahafidhina mambo leo nchini Marekani katika kipindi cha Bush mtoto na uvamizi wa Marekani dhidi ya Irak mwaka 2003 misukumo ya zamani ya Marekani imerudi kuisukuma Iran, lakini mara hii ni kwa kiwango cha chuki za kimadhehebu. Na hayo ni kwa kuzingatia mipango ya Marekani katika kurejesha mchoro mpya wa mipaka ya Sykes – Picot kwa kuzirarua nchi kivitendo juu ya msingi wa kimadhehebu hata zikibakia zipo kiumbo. Marekani ikazungumza kuhusu ramani mpya ya Mashariki ya Kati. Na Iran ikaanza kuyaunga mkono makundi ya kimadhehebu kwa ajili ya kupata mipaka mipya iliyochorwa kwa damu kwa ajili ya ramani za kimadhehebu za Marekani kwa Mashariki ya Kati. Na mipaka ya kimadhehebu ikadhihiri wazi wazi nchini Irak, kisha ikafka Yemen, Syria,Lebanon,Saudia, Bahrain, Pakistan, Afghanistan na nyenginezo, baada ya kuwa Iran imenyanyua mwito wa "Jamii ndogo", yaani ilikuwa inatekeleza siasa ya kuhifadhi jamii ndogo inayopigiwa debe na Marekani. Na hapa ndipo ilipodhihiri dori ya Iran kwa kasi.

b-**Ama Misukumo Mipya Na Ya Dharura,** ni "Vugugu la Warabu", Marekani imejikuta yenyewe mbele ya jambo la kujitosa(hatari) na jipya. Ghasia za vugugu la Warabu zimezuka ghafla nchini Tunisia, Yemen, Misri, Libya na Syria, na Marekani haikua ni yenye matayarisho ya kulinda ushawishi wake mbele ya mapinduzi haya ya raia ambayo yalitishia kuvunja ushawishi huo. Na Marekani haiwezekani kutuma jeshi lake kulinda ushawishi wake kwasababu ya kile ilichokipata jamii ya Marekani

*Endelea Uk..13*

kuhusu uzito(wa vita vya) Iraki. Na haina jeshi la kieneo ambalo linaweza kulinda ushawishi wake kiukamilifu,

Basi vibaraka wake muhimu zaidi katika eneo – Misri na Syria wakawa chini ya moto wa machafuko na mapinduzi. Kwahiyo Marekani ikakuza misukumo mipya ya dharura kwa haraka ya kulazimika kuitegemea Iran kwa kiasi kikubwa, na Iran ikazuka ikashambulia mapinduzi nchini Syria hasa na inazidi kukitia nguvu chama chake cha Lebanon ili kuzuia mapinduzi yasiivunje Lebanon pia baada ya matukio ya Tripoli na Sidon. Na ikazidi kuwatia nguvu wafuasi wake katika Bahren na Yemen ili kufikia ushawishi wa Marekani humo kwa matumizi ya Marekani. Yote haya ni kutokana na hali halisi ya mapinduzi na kwa misukumo hii mipya ya Marekani, dori ya Iran yenye maumbile ya kimadhehebu imekuwa kubwa na ya kutisha sana katika eneo. Na siasa hii ya Marekani imepelekea kudhihiri ukuruba wa wazi wa Marekani – Iran. Vyombo vya habari vimezungumzia juu ya usafirishaji wa fedha kwa ndege kwenda Iran baada ya maafikiano ya nyuklia, mikataba ya kibiashara na kampuni ya Boeing, kukutana kwa maofisa wa Marekani na mabenki ya Ulaya ili kurahisisha miamala na Iran na kuondoa khofu za mabenki kutokana na vikwazo vya Marekani…

3-Na kwa kurejea Saudia katika milki ya Marekani baada ya kufa Abdallah aliye mtiifu kwa Muingereza na kuchukua utawala kibaraka wake Salman na mwanawe nchini Saudia mwaka 2015, na kuchukua Al-sisi urais mwaka 2014 wamepata nguvu vibaraka wa Marekani katika eneo na imepata uwezo wa kulinda ushawishi wake bila ya Iran pia. Huu ni upande mmoja… Na upande mwengine Marekani imeona udhaifu wa Iran,

Kwasababu haikuweza pamoja na wanamgambo wake wote na walinzi wake na msaada wake kuvunja nguvu za mapinduzi ya Syria, Marekani sasa ikaivuta Urusi kwenda Syria lakini Urusi haikua badili ya dori ya Iran bali ni kuitegemea. Yote haya yamefungua muono kwa Wshington kufikiria aina kadhaa za nyenzo za siasa zake. Na kwamba kuitehemea kwa nguvu sana na namna fulani ya kipekee Iran haikua na athari…

Na kwa kukaribia mwisho utawala wa kipindi cha pili cha Obama funguo za kudhibiti mapinduzi ya Syria zilikua zinakusnyika kwa Uturuki Marekani ikazikusanya siasa mbili ya usambaratishaji, kwa “Iran na Urusi” na siasa ya udhibiti, kwa “Uturuki” ili kuvunja nguvu ya mapinnduzi ya Syria. Kisha dori ya Saudia kuwaliwaza wapinzani Riyadh!

Hivi ndivyo ilivyo, basi dori ya Iran katika eneo ni siasa ya Marekani iliyopangwa kwa uthabiti. Na dori hii hutanuka na kunywea kulingana na matakwa ya siasa ya Marekani na kulingana na dhurufu. Na tangu mwaka 1979 Marekani imekua ikiihifadhi Iran kama ni kitisho “Cha kimapinduzi kwa guo la Uislamu” dhi ya nchi(zote) za eneo. Kisha hayo yakapanuka kuwa “kitisho kikubwa cha kimadhehebu” baada ya kupata utawala wahafidhina wapya Marekani, kisha ikawa “dori muhimili ya kieneo” ambayo ina uzito wake dhurufu za vuguvugu la Warabu. Lakini iliporejea afya kwa baadhi ya vibaraka wa Marekani wengine mfano nchini Misri, au kurejea kwa utawala katika mkono wake kama nchini Saudia, au kuwa uwezekano wa kuitumia kama Uturuki, Marekani inatafuta dori nyengine kando na dori ya Iran bila ya kuiacha hiyo(Iran).

Na inapasa kusema kwamba dori ya Iran katika eneo ni kama dori ya vibaraka wengine wa Marekani, na haiwakilishi ushawishi wa kikweli wa Iran na wasiokua Iran katika wafuasi wa Marekani. Na Marekani huzidisha na kupunguza dori hizo bila hata kuzingatia maslahi ya nchi hizo… Kwa mfano Iran inatumia kwa ajili ya Syria karibu na kuimaliza hazina yake bila ya kuangalia miundo mbinu yake inayochakaa, na inaelewa kwamba inawezekana Marekani kumaliza dori yake nchini Syria itakapoona haiihitajii tena!

Na vilevile Marekani imezaa dori ya Saudia nchini Yemen ambayo imeiudhi sana Iran mbele ya wafuasi wake, kwa kule kudhihirika wazi Saudia ndiyo inayotoa msaada wa kijeshi moja kwa moja kwa wafuasi wake, katika wakati ambao Iran imeitambua hasa dori ya Saudia na namna ilivyo na nguvu juu hali ya Yemen na Iran ikawa imedhalilika nyuma ya marikebu ndogo zinazosafirisha silaha kwenda kwa Mahouthi… Na huenda katika kufuatilia dori ya Uturuki nchini Syria na kuanguka kwa mistari myekundu bali na kubadilika kwa lugha ya kauli zake na misimamo yake ni mambo ambayo yanadhihirisha kwa kiasi gani Marekani katu haiwajali viongozi hawa, inawadhalilisha na kuwachukiza bila ya kupwesa! Yaani Marekani inazidisha na kupunguza dori ya wafuasi hao(vibaraka) kwa hali endelevu na kulingana na maslahi yake yeye bila ya kuwajali wao.

**Siasa Ya Marekani Kuelekea Iran Baada Ya Trump:**

Katika mazingira haya ya Marekani kuzipa dori nchi nyengine zisizokua Iran katika eneo, nazo ni Uturuki na Saudia na kudhoofisha dori ya Iran. Katika mazingira haya ndio Trump akachuka uongozi wa White House. Na ilikua inawezekana siasa ya Marekani kuendelea na mbinu zilizotangulia kuelekea Iran bila ya kokoro na kuendelea nchi tatu za kieneo katika kuitumikia Marekani kila moja kulingana na dori yake… Lakini Trump alitaka kushughulisha utisho wa Iran kwa kuiharibu kiuchumi kwa njia ya ‘kimafia’ ambayo inapendwa na Trump,kwahiyo akawa anachochea hali tete na Iran, akaishambulia kwa njia ya twita (twiter) akaiita kuwa inadhamini ugaidi. Na akaituhumu kuwa ina itisha Marekani na waitifaki wake na akadhihirisha ukeketevu katika kuamiliana nayo. Na akaweka vikwazo zaidi kwa watu 25 na makampuni nchini Iran tarehe 3/2/2017 baada ya majaribio yake ya makombora. Na akayaelezea maafikiano ya kinyuklia kuwa kuwa mabaya , na akadokeza uwezekano

*Endelea Uk..14*

wa kuyapitia upya na kuyafuta, yaani kuitoa Marekani kutoka makubaliano hayo. Na hapa ndio baadhi ya watu wakadhani kuwa Trump anafanya mabadiliko makubwa katika siasa za Marekani. Na ili tufahamu mtazamo "mpya" wa Trump kwa Iran na dori yake na kiasi ambacho yawezekana Trump akafanya kwa Iran, tunaachunguza mambo yafuatayo:

1-Kwamba siasa ya Wa-republican inategemea kudhihirisha nguvu na ubabe. Hili liko wazi katika kila kigezo cha siasa za nje za Trump ikiwemo inayohusiana na Iran.

2-Naam, kuna jambo jipya katika mtazamo wa Marekani – Trump kuelekea Iran. Na muktadha wa jambo hili ni kwamba rais Trump aliahidi kutatua mambo mengi ya kiuchumi kwa Marekani. Na alitaka waziwazi mataifa ya ulimwengu yagharamike kwa ajili ya Markani kwa kule kuyalinda kutokana na hatari, na iliijumuisha hilo jambo jiipya Japan, Korea, mataifa ya Ulaya ya Atlantic(Atlantic Europe) na mataifa tajiri ya ghuba hayakuachwa, bali ndio mawindo mepesi. Na kwa yale yaliyotajwa katika misukumo ya Marekani ya zamani na mipya kuwa imenyanyua umuhimu wa Iran na dori yake katika eneo la ghuba, na kwamba utisho wa Iran katika kipindi cha Obama umekua ni hatari kubwa kwenye milango ya (nchi za) ghuba, basi hakika rais Trump anataka kuwekeza kiuchumi katika jambo hili na kwa njia ya kimafia. Trump anataka kutia mkononi mapato makubwa ya mafuta kutoka nchi za ghuba kwa kuishinikiza Iran na kudhoofisha dori yake na kwa kuzilinda nchi hizo kutokana na hatari ya Iran. Kwa haya na mbele ya shinikizo hili la Marekani dhidi ya Iran, unaiona(Iran) inafanya majaribio ya makombora mapya. Na haliko mbali(kuamini) kwamba hilo lilikua kwa uratibu kamili wa Marekani na si ghafla tu kusadifiana na wakati, yaani inathibitisha hatari yake kwa mataifa ya eneo(la ghuba) bila ya yenyewe kupata faida kwa hilo, bali mwenye kupata faida ni Marekani ambayo leo inatafuta fedha nyingi kwa kuwalinda watawala kutokana na Iran. Na kauli za Trump katika kampeni yake ya uchaguzi zinathibitisha mpango huu. Na katika kauli ambazo zinaashira "fikira mpya" ya Trump ni haya yafuatayo:

-Ilieleza CNN ya Kiarabu tarehe 19/8/2015 kuwa Donald Trump anaitaka Saudia kutoa mali kuipa Marekani kwa ajili ya kuilinda isisambaratishwe, akasema: "Saudia karibuni hivi itakua katika tatizo kubwa na itahitaji msada wetu… lau kama si sisi isingekuwepo na isingebakia".

-Na tukinukuu tovuti ya CNN ya Kiarabu tarehe 27/9/2016, Trump alisema: "Tunailinda Japan. Tunailinda Ujerumani. Tunailinda Korea ya Kusini. Tunailinda Saudia. Tunazilinda nchi kadhaa, wala hazitulipi (kwa hilo) chochote. Lakini inahitajika watulipe kwasababu tunawapatia huduma kubwa na tunapoteza mali nyingi… Yote nisemayo ni kwamba la kulishika zaidi ikiwa wao hawakutoa sehemu yao stahiki…Wanalazimika kujilinda wenyewe au iwalazimikie msaada wetu. Sisi ni taifa lenye deni linalofikia trilioni 20, inawalazimu msaada wetu". Na Trump akaongeza kwa nguvu umuhimu wa "uwezo wa mazungumzo katika maafikiano ya kimaslahi ya kibiashara". Akaeleza: "Lazima uwe na uwezo wa mazungumzo na Japan na Saudia. Ninyi ndio munadhania kwamba tunailinda Saudia? Kwa mali zote ilizonazo, sisi tunailinda na wao hawatulipi chochote?"

-Tovuti ya Aljazeera ilisema tarehe 26/1/2017 "Rais wa Marekani alisema kwamba Iraki ilikua inamiliki nguvu zinazolingana na Iran isipokuwa Marekani ilifanya kosa ilipoingia Iraki – katika kuashiria vita ya Marekani dhidi ya Iraki mwaka 2003 – kisha ikazikabidhi kwa Iran, akiashiria kwamba uongozi wa Marekani ulipaswa kusalia huko na kuhodhi mafuta ya Iraki". Na kama ilivyonukuu tovuti ya Reuters ya Kiarabu tarehe 24/1/2017(Katika hotuba mbele ya maofisa wa CIA Trump alidokeza kwamba Marekani ilipaswa kuchukua mafuta ya Iraki kufidia mzigo wa vita mwaka 2003).

3-Yote hayo yanathibitisha yawezekanayo kuwemo katika akili ya Trump ambayo inatafuta kufanya makubaliano ya kimaslahi, basi badili kwa ulinzi wa vijidola vya ghuba kutokana na hatari ya Iran lazima zitowe gharama za ulinzi huo. Yaani kuweka fedha zake nyingi chini ya matumizi ya Marekani kwa ajili ya kuhifadhi viti vya utawala. Marekani ina amiliana na viongozi hawa kwa kuwachukulia kama ni watoto wadogo. Na akili hii ya kimafia ya uongozi wa Trump inathibitishwa na ushahidi kadhaa…Rais Trump si upande pekee wa Marekani uliojfunga na mapato makubwa ya kimataifa,

Congress ya Marekani imejifunga na sheria ya JUSTA mwaka 2016 katika kipindi cha utawala wa Obama na ikawa inawezekana kwayo kuzuia fedha za Saudia na nchi nyengine za ghuba kwasabau ya vtendo vya "kigaidi"… Na hayo ni kwasababu Marekani ina mizozo ya kiuchumi hasa inayoilazimisha kupunguza bajeti yake kijumla na mbele ya madeni makubwa iliyonayo, na kuinuka kwa uchumi wa China. Ndio ikawa(Marekani) siku zote inatafuta masuluhisho makubwa, ndipo ulipoona uongozi wa Bush mtoto kuwa utatuzi wa kiuchumi ni kuitawala Iraq na kufaidika na mafuta yake,

Lakini upinzani nchini Iraq ulimzuia hivyo, akalazimika kutumia dola trilioni 3 kwa janga la Iraki. Obama akajaribu kupiga kodi murua (tax havens) ya Uingereza ili kuvutia fedha nyingi kutoka visiwa vya mbali kwenda Marekani. Kisha sheria ya JUSTA ikaja ili kupata fedha za kodi na kugharimia "ugaidi". Na sasa Trump anazitaka nchi tajiri za ulimwengu zilipe mapato ya kimataifa kama ni badili ya kuzipa ulinzi ili kutataua kizungumkuti cha uchumi wa Marekani. Na Trump anagubikwa na ahadi yake ya kutatua deni la Marekani(dola trilioni 20) katika kipindi cha miaka minane!

4-Hakika ya miito aliyokuwa akiimba

*Endelea Uk..15*

Trump “Kuirejesha Marekani kuwa dola kubwa mara nyengine” inapelekea Marekani kuingilia moja kwa moja, na kukataa siasa ya Obama kujificha nyuma ya dori(inazowapa) wengine, kama ulivyojaribu uongozi wa Trump katika kauli za maeneo salama nchini Syria ni kurejesha dori yake moja kwa moja kwa kuichukua kutoka Urusi. Na dori kubwa na ya kuogofya iliyopewa Iran katika muktadha huu imekuwa inayofata kutizamwa upya vile vile.

Kwahivyo uongozi wa Trump umefikiri kwa makini katika kupunguza dori ya Iran baada ya kumalizika kwa lengo la kiuchumi katika hilo, lakini bila ya kuwa kutoihitajia ili iwe dori yenye kukamilisha dori ya Uturuki na Saudia na sio kuwa badili yao, yaani haina(Iran) dori ya kuongoza na hasa nchini Syria, bali inarudi chini sana dori yake mbele ya dori ya Uturuki kimsingi na kisha dori ya Saudia. Lakini dori ya Iran inabakia ipo kutumikia mipango ya Mareakni. Basi Marekani haiwezi ikajitosheleza na dori hii katika eneo.

5-Kwahivyo, hukmu ya mas-ala ya Marekani kubadilisha dori ya Iran haijengwi juu ya kauli na hotuba kama inavyojengwa juu ya vitendo. Kwani makelele leo yanayopigwa na Washington kuhusu Iran mengi hayafikii daraja ya kufanya mabadiliko. Kwa mfano(Alitamgaza rais wa Iran, Hassan Rohani katika hotuba aliyoitoa katika sherehe za kumbukumbu ya 38 ya mapinduzi ya Iran, kwamba Wairan wataifanya Marekani ijutie matamshi ya vikwazo. Rohani akaashiria kwamba kushiiriki kwa Wairan katika kuhuisha kumbukumbu ya “Mapinduzi ya Kiiislamu” ni kuonesha nguvu za kitaifa Nyanja kadhaa nchini. Akielezea kwamba kushiriki huku ni ujumbe wazi unaojibu kauli za viongozi wa White House). (Russia Today, 10/2/2017).

Huku akijibwa na Rais wa Marekani, Trump, kwa kauli yake “Chunga” (Siku ya Ijumaa rais wa Marekani Donald Trump alimwambia rais wa Iran ajihadhari, hayo ni baada ya yale yaliyonukuliwa na vyombo vya habari kuhusu tamko la Rohani kwamba mtu yeyote anayetishia Wairani atajuta. Akasema Trump: “Chunga. Ni bora kwako”) (Reuters, 10/2/2017). Haya na yanayofanana nayo miongoni mwa kauli ni kama yale maafikiano ya nyuklia yote yanaangukia kwenye rekodi yenye kuchosha ya mpambano wa Mrekani – Iran… Ama hali halisi uwanjani ni uratibu, mashirikiano, na utekelezaji wa mipango ya Marekani,

(Mugireny aliwaambia waandishi wa habari baada ya mikutano yake na maafisa wa ofisi ya rais wa Marekani Donald Trump, siku ya tarehe 9 Februari ifuatavyo: “Kwa mujibu wa yaliyosemwa katika mikutano ile nimethibitishiwa azma yao ya kujifunga katika kutekeleza maafikiano ya kinyuklia na Iran kikamilifu”) (Russia Today, 10/2/2017). Ama vikwazo vipya vilivyowekwa na Mrekani dhidi ya Iran bado viko katika mtazamo mdogo, ijapokua vimewekwa sambamba na kauli zinazoelekeza kwamba Marekani inapitia upya dori ya Iran, lakini inaipitia kwa kuzingatia kuwa ndio siasa yake. Inapitia mafanikio yake na kasoro zake, na vipi itawezekana kuitumia kwa faida ya kiuchumi na kisiasa kwa maslahi makubwa ya Mareakni.

Kuipitia upya dori ya Iran si kioja kwa Trump tu, bali mgombea wa Democrat, Hillary Clinton alikuwa akieleza hayo ya kupitia upya katika kampeni zake za uchaguzi. Aliieleza siasa ya “Uaminifu na Uthibitisho” inayoshikwa kuelekea Iran kuwa “Sio siasa nzuri” na kwamba yeye badala yake atategemea siasa ya “Kutoiamini Iran”. Na akaahidi kurejeshwa kwa vikwazo dhidi ya utenguzi wowote hata mdogo wa maafikiano ya nyuklia bali hata kutumia nguvu za kijeshi dhidi yake ikiwa kuna hali ya utenguzi wa maafikiano (Al-Sharq Al-Awsat, 22/3/2016). Yaani uongozi wa Trump kupitia upya dori ya Iran ni siasa ya nchi ya Marekani.

**Mwisho, ni jambo la aibu** kuwa Marekani ambayo inaozeshwa na funza kutoka ndani ambayo ni natija ya hadhi zake fisidifu na hadhara yake chafu. Ni jambo la aibu kuwa hii(Mareakni) kuwa na ushawishi katika biladi za Waislamu ikijitapa humo. Na huku wanaojiita wenyewe viongozi wakishindana katika kuitumikia!! Na katika jambo linaloumiza sana ni miji ya waislamu kuwa ndio medani ya mipango ya makafiri wakoloni! Lakini sababu inajulikana, tuliisema na tunairejea… Ni kukosekana kwa Khalifah, kiongozi ambae ni ngao. Kutoka kwa Abuu Huraira, kutoka kwa Mtume (saw) amesema: **“Hakika kiongozi ni ngao. Hupiganwa nyuma yake, na hujikinga kwake”** Muslim.

Lililowajibu juu ya kila Muislamu anaempenda Allah na mjumbe wake liwe jambo hili ni la kufa na kupona: Kufanya kazi kwa bidii ya dhati na ikhlas kwa Allah Aliyetakasika na kwa uaminifu pamoja na mjumbe wake (saw). Na halo ni kwa kusimamisha Khilafah Rashida, ithibiti bishara ya Mtume mkarimu baada ya utawala huu(uliopo) wa kidhalimu, kama ilivyokuja katika hadithi sahihi iliyopokelewa na Ahmad na Twayalisy, na maneno ni ya Twayalisy: Amesema Hudhaifah: Kasema mjumbe wa Allah(saw): “… **kisha utakua (utawala) wa kidhalimu, utabakia mpaka muda autakao Allah. Kisha atauondosha atakapo kuuondosha. Kisha ikua (itarudi) Khilafah kwa njia ya Utume”**… Na hapo wapate nguvu na wadhalilike makafiri wakoloni na waihame miji ya Waislamu wende kwenye uti wa mgongo wao kama ukibakia huo uti wa mgongo wao. **“Na hayo ni masiku tunayoyabadilisha baina ya watu. Na ili Allah awadhihirishe wale walioamini na awafanye miongoni mwenu mashahidi. Na Allah hawapendi madhalimu”**

**26 Jumada1 1438H**
**23 Februari, 2017M**